

Wapendwa wasomaji wetu, nilazima tujuwe ya kwamba: Sio vizuri Kuwabagua watu katika dini zetu, huku tukifahamu yakuwa, wakati mwengine UBAGUZI KATIKA DINI huleta matengano pia huchochea chuki kati ya wafuasi. Kwake Yesu hapana Myahudi wala Myunani, bali sote tumekuwa wamoja katika Kristo Yesu *(Wagalatia 3 :28)*. Tuko wana wa Baba mmoja pia imani moja. Nakazalika, UBAGUZI KATI YA DINI KWA DINI husababisha ugonvi mkubwa kati ya watu, kama tulivyo soma katika kitabu hiki. Hizo ni hasara kubwa. Mambo haya yote ni machukizo kwake Mungu kwani yeye ni mpatanishi, kwake yeye hakuna hata haina moja ya UBAGUZI. Mungu Baba ni UPENDO, na Upendo hauna ubaguzi. Kwahiyo, wapendwa tujitenge sana na hayo, kwa kuhepuka kuleta UBAGUZI KATIKA DINI wala UBAGUZI KATI YA DINI KWA DINI, tusije tuka sababisha hasara kubwa katika jamii.




Ndugu zetu wapendwa wasomaji wa vitabu vyetu, tunawasalimu mara tena. Tuna waletea kitabu hiki cha pili, ambacho kinazungumzia kuhusu " UBAGUZI NDANI YA DINI " pia " UBAGUZI KATI YA DINI KWA DINI". Ukweli uliopo ni kwamba, nyakati hizi watu wengi walio katika dini moja, wana baguana wao kwa wao. Wamoja ambao ni matajiri wabaguana na wa maskini, wengine wajionao kuwa wakiroho hujibagua na wengine wanao onekana kuwa wakimwili... Hata wengine wanao jiita kuwa ndio wa kabila la waanzilishi wa dini fulani, wana bagua wengine ambao sio wa kabila lile. Kwahiyo, hawa watu hao wa kabila lililo anzisha dini hiyo wajiona kuwa dini hiyo ni kitu chao, hawawezi kamwe kukubali mtu yeyote wa kabila lingine apewe cheo kikuu katika dini yao hiyo. Pia katika kitabu hiki, tutaona jinsi dini zimoja zina kataa kabisa kushirikiana na dini zingine, wala hata kusalimiana na wafuasi wa dini zingine ambazo wameona kuwa ni dini isio faha, ni dini zaki shetani. Karibuni, twawatakia usomi mwema.

**Jumapili mojawapo, wafuasi wa dini inayoitwa 98ème COROLA, wamekusanyika hekaluni pao ili kumuabudu Mungu wao. Walipo kuwa wame endelea na ibada yao, papo hapo, mama mmoja anaitwa kuwa ni nabii miongoni mwao, akaanza kutabiri kwa sauti kubwa...**






**Kwa masikitiko makubwa na huzuni nyingi mchungaji KATY, wa kabila la wa Jonchuwan, anatangaza rasmi kulitowa hekalu lake katika dini ya 98ème COROLA, ambayo viongozi wakuu wao wamejaa UBAGUZI.**



**SALOMON, mchungaji mmoja wa kabila la waswahili anamkumbatia kwa kutaka kumfariji KATY, mchungaji mwengine wa kabila la Jonchuwan, huyu hataki kufarijika pia ana mjulisha mwanziwe kwamba, wafuasi wa kabila lao wote watatoka katika dini yao ya $98^{\text{ème}}$ COROLA na kuunda dini nyingine.**






**Baada ya mama yule nabii kumaliza kutabiri, mchungaji mkuu katika hekalu hilo akasimama kwenye mazabau nakuanza kutangaza mbele za wafuasi wao, huku akikazia yale ambayo nabii yule alikuwa akiyatabiri.**



**Mchungaji huyo ana endelea kukazia sana kuhusu unabii ulio tolewa na mama yule, hekaluni.**







**Furaha ya wamoja ni huzuni ya wengine. Matokeo ya uchaguzi wa Askofu mkuu wa dini ya 98ème COROLA, yame huzunisha sana watu wote wa kabila lawa Jonchuwan waliokuwa wafuasi katika dini hiyo. Mwishowe watu wa kabila hilo walichukuwa maamuzi ya kutoka katika dini hiyo.**



**Msimamizi mkuu kiongozi wa baraza la uchaguzi anatangaza matekeo ya mwisho, ya uchaguzi wa Askofu mkuu wa dini ya 98ème COROLA.**






**Wachungaji, wakuu viongozi wa dini ya 98ème COROLA wamekutana pamoja kwa ajili ya mazungumuzo kuhusu kubaguana na dini zingine ambazo wameona kuwa ni dini zisizo faha, azielekei kwenye ma aadili yaki Mungu.**




Siku chache baadaye, mchungaji wa kanisa moja wapo wa dini ya 98ème COROLA akasimama mazabahuni na kutangaza yale ambayo wamekubaliana katika kikao, siku ile.






Wakiwa tayari katika baraza; baada ya kufanya uchaguzi wa Askofu mkuu wa dini ya 98ème COROLA, watu wote wakaa kimya kwa utayari waku sikiliza matokeo ya uchaguzi huo, na huku msimamizi mkuu kiongozi wa kikao hicho ana anza kutangaza hayo matokeo ya uchaguzi.



**Walipo maliza ku jadiliana, wote waka simama naku jielekeza katika baraza la uchaguzi. BONY akawa mwenye furaha kubwa pia tumaini lakuchaguliwa, kwakuwa kabila zingine zime baguliwa, kwahiyo hana mpinzani mwengine.**






**Kwaajili ya ubaguzi wa dini kwa dini, wafuasi wa dini ya 98ème COROLA wana gombana njiani pamoja na wafuasi wa dini nyingine, kwa sababu wamoja wame zarahu naku tukana wengine eti imani yao ime waelelkeza kuzimu sababu yaku ruhusu wanawake kuingia hekaluni wakivaa suruali, pia hawa vaaki vitambaa kichwani wanapokuwa waki hudumia.**



**Wakuu viongozi wote wa dini ya 98ème COROLA wamekutanana mahali pamoja kwa ajili ya uchaguzi wa Askofu wao wa mpya. Katika mazungumzo kwenye kikao hicho, msimamizi, mkuu kiongozi wa kikao hicho, ametangaza jambo moja ambalo lime chochea UBAGUZI MKUBWA kati ya makabila ya wafuasi katika dini hiyo.**






**Baadaye kidogo, watumishi wote walio wanamemba katika kikao hicho cha uchaguzi wa Askofu mkuu, wakatoka inje ya baraza la uchaguzi ili kujadiliana kuhusu kumchagua Kandideti wao atakaye gombea kuwa Askofu katika dini yao ya 98ème COROLA. Watu wana jadiliana wakiwa vikundi vikundi, wale wa kabila la waswahili wana mpendekeza BONY.**

